c) Kuzingatia matakwa ya kisheria kuhusiana na uandishi wa maelezo;

d) Kutomlazimisha mtuhumiwa kusema lolote isipokuwa kwa hiyari yake mwenyewe;

e) Kuzingatia ukomo wa muda wa uchukuaji wa maelezo ambayo ni masaa manne baada ya kufikishwa kituoni, hata hivyo sharti hili hutegemea mazingira;

f) Kuyasoma maelezo kwa mtuhumiwa au kufanya maelezo hayo yasomwe kwa mtuhumiwa, au kumpa mtuhumiwa asome maelezo aliyoyatoa.

## 7.1 Athari Za Kutozingatia Utaratibu Wa Uchukuaji Wa Maelezo

Ikiwa maelezo ya mtuhumiwa yatachukuliwa pasipo kuzingatia utaratibu na haki zilizoainishwa kisheria , maelezo yaliyotolewa hukosa uhalali wa kutumika Mahakamani kama ushahidi wa kuthibitisha kosa la mshitakiwa hasa pale inapotokea kuwa mtuhumiwa amekiri tuhuma zinazomkabili.

## 8.1 HITIMISHO

Maelezo ya onyo ni moja ya hatua katika mfumo wa haki jinai kwakuwa hatua hii inatoa nafasi kwa mtuhumiwa kushirikiana na vyombo vya upelelezi. Mtuhumiwa kuchukuliwa maelezo kuhusiana na tuhuma zinazomkabili kunasaidia vyombo vya upelelezi kupata maelezo kutoka kwa mtuhumiwa kuhusu suala analotuhumiwa nalo.
Vilevile mtuhumiwa anakuwa amepata haki ya msingi ya kusikilizwa kuhusiana na tuhuma zilizowasilishwa dhidi yake.

---

**Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuwani ifuatayo:**


Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na.1
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA - TANZANIA

tumesheria.tanzania | www.lrct.go.tz
@tumesheria | TumesheriaTv


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



# HAKI ZA MTUHUMIWA ANAPOCHUKULIWA MAELEZO

## HAKI ZA MTUHUMIWA ANAPOCHUKULIWA MAELEZO

### 1.1 Utangulizi

Tume ya Kurekebisha Tanzania ilianzishwa mwaka 1980 kupitia Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kufanya tafiti za sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia.

Tume pia inajukumu la kufanya tathmini za utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini kama malengo ya kutungwa kwa sheria hizo yanafikiwa. Tume vilevile ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma ili kuweza kuwajengea wananchi uelewa wa sheria mbalimbali na hivyo kusaidia wananchi kushiriki kikamilifu katika maboresho ya sheria.

### 2.1 Maelezo ya Mtuhumiwa

Baada ya kukamatwa mtuhumiwa huchukuliwa maelezo na wapelelezi kuhusiana na tuhuma zinazomkabili. Utaratibu na haki za kuzingatiwa wakati wa uchukuaji wa maelezo zimeainishwa katika sheria mbalimbali kama vile Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Dawa ya Kulevya, Sura ya 95; Kanuni za Jaji Mkuu kuhusiana Uchukuaji Maelezo ya Watuhumiwa kwa Njia Sauti na Video za Mwaka 2023, na Amri za Kudumu za Jeshi la Polisi Namba 236.

### 3.1 Maana Maelezo ya Onyo

Maelezo ya onyo ni maelezo ambayo hutolewa na mtuhumiwa wa kosa la jinai baada ya kuwa amejulishwa na afisa anayemhoji kwamba halazimiki kujibu maswali anayoulizwa tofauti na yale yanayohusu utambulisho na anwani yake na endapo kama mtuhumiwa ataridhia kuyatoa basi maelezo hayo yanaweza kutumika kama ushahidi mahakamani dhidi yake. Maelezo ya onyo yamejengwa katika misingi ya hiari ya mtuhumiwa.

### 4.1 Namna ya Uchukuaji wa Maelezo ya Mtuhumiwa

Uchukuliwa wa maelezo ya mtuhumiwa akiwa katika kituo cha polisi huweza kufanywa kwa njia zifautazo;

a). Njia ya maandishi;na
b). Njia ya sauti na video.

### 5.1 Haki za Mtuhumiwa Wakati wa Uchukuliwaji wa Maelezo

Sheria imeainisha haki za mtuhumiwa wakati wa uchukuaji wa maelezo, haki hizo ni pamoja na;

a) Kujulishwa kosa analotuhumiwa;

b) Kutolazimishwa au kushurutishwa kusema lolote isipokuwa kwa hiyari yake mwenyewe. Hata hivyo mtuhumiwa anawajibika kutoa utambulisho wake na anwani yake;

c) Kupewa utambulisho wa askari anayemhoji;

d) Kutumika kwa lugha ambayo inaeleweka kwa mtuhumiwa;

e) Kupewa onyo kwamba atakayoyasema yanaweza kutumika mahakamani kama ushahidi dhidi yake;

f) Kumwita wakili wake, jamaa au rafiki yake wakati maelezo yake yanapochukuliwa;

g) Kuamua kama anataka kuandika maelezo yeye mwenyewe au mpelelezi kurekodi atakachokisema;

h) Kuthibitisha maelezo aliyoyatoa kama yameandikwa kwa usahihi kama alivyowasilisha;

i) kurekebisha maelezo yake mara baada ya kuyasoma au kusomewa;

j) Kama maelelezo yatachukuliwa kwa njia ya sauti au video atapaswa kujulishwa kuhusiana na hatua hiyo pia kuhakikisha kuwa vifaa vinavyotumika kurekodi maelezo yake havina maudhui mengine.

### 6.1 Wajibu Wa Afisa Anayechukua Maelezo

Sheria imeainisha wajibu wa Afisa anayechukua maelezo kutoka kwa mtuhumiwa kuzingatia yafuatayo;

a) Kuhakikisha anamfafanulia mtuhumiwa haki zote anazostahili katika zoezi la uchukuaji wa maelezo ya onyo;

b) Kuandika maelezo yaliyotolewa na mtuhumiwa kwa usahihi kama yalivyotolewa na mtuhumiwa;